

Genomic Selection Project

Kukidhi mahitaji ya wakulima wa baadaye kwa aina ya maharagwe

Ni kwa jinsi gani njia hii inayotumia maarifa ya genomic inaweza kuongeza uzalishaji wa mazao kwenye mashamba yanayomilikiwa na wanawake, wanaume, na yanayomilikiwa kwa pamoja katika mazingira tofauti?

Ni kupitia kuongezeka kwa uzalishaji, kipato, usalama wa chakula na lishe, na kuongeza maamuzi yanayojumuisha zaidi kwenye mashamba na nyumbani.

Hivyo basi, wakulima wenye vigezo vifuatavyo walichaguliwa: Angalau akiwa na miaka 4 ya uzoefu katika kilimo cha maharagwe; akiwa na umiliki wa ardhi au uwezo wa kupata ardhi; akiwa na utayari wa kushiriki; akiwa na maono kwenye maswala ya ushirikishwaji (kipato, umri, jinsia); na akiwa anaweza kutoa nafasi fulani katikati ya shamba.



Ugunduzi wa mbegu mara nyingi hufanyika kwenye vituo vya utafiti na sio mashambani kwa wakulima.



Ugunduzi wa mbegu wa njia ya kawaida huchukua miaka 8 hadi 12, wakati ugunduzi wa kutumia njia za genomics kupitia mashamba ya wakulima huchukua muda mfupi zaidi.




Wanaume na wanawake wana uchaguzi tofauti na mara nyingine wanaweza kuwa na uchaguzi unaofanana juu ya sifa fulani za mbegu, kwa hivyo tunahitaji kuelewa nani anapendelea nini?



Wakati mwingine wanawake hawapewi nafasi ya kuelezea machaguzi yao au sifa za mbegu wanazozitaka. Kwenye hili tunawajumuisha.

Tuliweza kufikia malengo ya asilimia 30 kwenye mashamba yanayosimamiwa na wanaume, asilimia 30 yanayosimamiwa, na asilimia 40 yanayosimamiwa kwa pamoja.



Tulianza na mashamba ya majaribio 93, kila mkulima alipata mbegu aina 3 za majaribio: zenye ukubwa wa kati, kubwa aina ya rosekoko, njano na nyekundu.



Wakulima wanatarajiwa kufanya usimamizi wa kawaida kwenye maeneo haya wanayotoa kwenye mashamba yao. Na pia wanatarajiwa, kupata ushauri kutoka kwa wanashauriwa na maafisa ugani. Kwasababu ya uongezeko wa mabadiliko ya hali ya hewa nchini, wakulima walipendelea mbegu za majaribio ambazo zinafaa kwa hali ya hewa na zilizokuwa na ustahimili wa mvua nyingi au ukame na joto.



MORE INFORMATION

Gender-responsive genomic selection on farmers' fields for accelerating genetic gains